Arusha, Tanzania

Tovuti: [www.african-court.org](http://www.african-court.org)

Simu: +255-272-510-510

AfCHPR
African Court on Human and Peoples' Rights

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**ELINAZI ELIABU *KWA JINA JINGINE* MSHANA**
**DHIDI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OMBI NAMBA 060/2019**

**HUKUMU KUHUSU USTAHILI NA FIDIA**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Mjini Arusha, tarehe 6 Machi 2026**: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) ilitoa hukumu katika kesi ya *Elinazi ELIABU kwa jina jingine MSHANA dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

Elinazi Eliabu *kwa jina jingine* Mshana ("Mwombaji") ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Taifa Lililoshtakiwa). Wakati wa kuwasilisha Ombi hili, alikuwa amefungwa katika Gereza la Ruanda, at Mbeya, akitumikia kifungo cha miaka 30 baada ya kesi yake kusikilizwa na kupatikana na hatia na kuhukumia kwa hatia ya unyang'anyi wa kutumia silaha. Anadai kwamba kulikuwa na ukiukaji wa haki zake wakati wa kukamatwa kwake na alipokuwa mbele ya mahakama za kitaifa.

Taifa Lililoshtakiwa lilipinga mamlaka ya Mahakama pamoja na ukubalifu wa Ombi hili.

Kuhusu mamlaka ya Mahakama, Taifa Lililoshtakiwa lilizua pingamizi kuhusu mamlaka ya Mahakama kusikiliza kesi zenye madai ya kukiukwa kwa haki za binadamu. Hususan, Taifa Lililoshtakiwa lilidai kuwa Mahakama hii linachukua jukumu la kufanya kikao kama mahakama ya rufaa, wakati haina mamlaka hayo. Kwa mujibu wa Taifa Lililoshtakiwa, Mwombaji alikuwa anaiomba Mahakama hii kufutilia mbali maamuzi ya mahakama za ndani za Taifa Lililoshtakiwa, huku haina mamlaka ya kufanya hivyo.

Kuhusu dai kwamba Mahakama itakuwa ikitekeleza mamlaka ya rufaa, Mahakama ilieleza falsafa yake ya sharia kuonesha kwamba haitekelezi mamlaka ya rufaa kuhusiana na madai ambayo tayari yamechunguzwa na Mahakama za kitaifa. Hata hivyo, wakati huo huo, na ingawa si mahakama ya rufaa ikilinganishwa na mahakama za ndani, inayo mamlaka ya kukadiria uhalali wa kesi za ndani dhidi ya viwango vilivyowekwa katika hati za kimataifa za

haki za binadamu zilizoidhinishwa na Taifa linalohusika. Katika kutekeleza kazi iliyotajwa hapo juu, Mahakama ilishikilia kwamba kwa kufanya hivyo haiwi mahakama ya rufaa.

Kuhusu pingamizi ya Taifa Lililoshtakiwa kwamba Mahakama hiyo haina mamlaka ya kubatilisha maamuzi ya mahakama zake za ndani, Mahakama ilirejelea Ibara ya 27(1) ya Protokali ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Uanishwaji wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu an Watu (Protokali), na kuhitimisha kuwa inayo mamlaka ya kutoa aina mbalimbali za fidia, pamoja na amri ya kubatilisha kesi zinazoendeshwa katika mahakama za kitaifa, amri ya kubatilisha upatikanaji wa hatia na hukumu yake, na kuamuru kuachiliwa kwa Mwombaji kutoka gerezani, mradi tu ukiukaji unaodaiwa umethibitishwa.

Mahakama ilibainisha zaidi kwamba madai ya ukiukaji yaliyowasilishwa mbele yake yanahusu haki zilizoelezwa katika Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu (Mkataba), ambao Taifa Lililoshtakiwa ni Mshirika, na kwamba ilikuwa na mamlaka inayofaa ya kusikiliza kesi za ukiukwaji wa haki za binadamu kuiwezesha kuchunguza Ombi hilo.

Kwa sababu hizi, Mahakama ilitupilia mbali pingamizi ya taifa Lililoshtakiwa kuhusu mamlaka yake ya kusikiliza kesi za ukiukaji wa haki za binadamu.

Ingawa vipengele vingine vya mamlaka yake havikupingwa na Taifa Lililoshtakiwa, hata hivyo, Mahakama ilivichunguza. Kuhusu hilo, Mahakama hii iliamua kwamba ina mamlaka juu ya watu binafsi kwa kuwa, tangu tarehe 29 Machi 2010, Taifa Lilioshtakiwa liliwasilisha Azimio lililoelezwa katika Ibara ya 34(6) ya ProtokaliI, ambayo inaruhusu watu binafsi kuwasilisha maombi mahakamani dhidi ya Taifa Lililoshtakiwa kulingana na Ibara ya 5(3) ya Protokli. Mahakama iisisitiza kwamba kujiondoa kwa Taifa Lililoshtakiwa kwenye Azimio lililotajwa, mnamo tarehe 21 Novemba 2019, hakukuathiri Ombi hili kwa kuwa kujoondoa kulianza rasmi tarehe 22 Novemba 2020 na kwamba Ombi hili liliwasilishwa tarehe 15 Novemba 2019, na hiyo ni kabla ya Taifa Lililoshtakiwa halijajondoa Azimio lake.

Mahakama pia iliamua kwamba ilikuwa na mamlaka ya muda kwa kuwa ukiukaji unaodaiwa ulitokea baada ya Taifa Lililoshtakiwa kuwa mshirika wa Protokali hii. Mwisho, ilitambua

kwamba ilikuwa na mamlaka ya kieneo kwa kuwa matukio yanayozungumziwa yalitokea katika eneo la Taifa Lililoshtakiwa, ambalo ni mshirika wa Mkataba na Protokali.

Mahakama ilisema kwamba kwa mujibu wa Ibara ya 6(2) ya Protokali, lazima ifanye uamuzi kuhusu ukubalifu wa kesi zote zilizofikishwa mbele yake. Kuhusu Ombi hili, Taifa Lililoshtakiwa lilitoa pingamizi kuhusu ukubalifu wa Ombi kulingana na kutotumia kikamilifu njia zote za usuluhishaji wa ndani.

RKuhusu pingamizi ya Taifa Lililoshtakiwa kwamba Mwombaji alikosa kutumia kikamilifu njia zote za usuluhishaji za ndani, Mahakama aliamua kwamba Mwombaji alikuwa ametumia kikamilifu njia zote za usuluhishaji wa ndani kwa kuwa Mahakama ya Rufaa ya Taifa Lililoshtakiwa, chombo cha juu zaidi cha mahakama katika Taifa Lililoshtakiwa, ilikuwa imekubaliana na upatikanaji wa hatia na hukumu ya mahakama za chini, kufuatia kesi ambapo Taifa Lililoshtakiwa lilikuwa na fursa kuzungumzia ukiukaji uliodaiwa na Mwombaji kuwa ulitokana na kesi na rufaa zake. Kwa sababu hii, Mahakama ilitupilia mbali pingamizi za Taifa Lililoshtakiwa kuhusu ukubalifu wa Ombi.

Mahakama ilisema kwamba hakuna pingamizi zilitolewa kuhusiana na mahitaji mengine ya ukubalifu, hata hivyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 50(1) ya Kanuni hizo za Mahakama (kanuni), ilikadiria vigezo vyote vya ukubalifu vilivyoelezwa katika Kanuni ya 50(2) ya Kanuni hizo, ambayo kimsingi inarejelea vifungu vya Ibara ya 56 ya Mkataba, ili kuhakikisha kwamba Ombi hilo linatimiza viwango vinavyotakiwa.

Kwa mantiki hiyo, Mahakama iliamua kwamba Mwombaji alikuwa ametambuliwa wazi kwa jina, kwa kutimiza Kanuni ya 50(2)(a) ya Kanuni hizo. Pia iliamua kwamba madai ya Mwombaji yalikusudia kulinda haki zake kwa mujibu wa Ibara ya 3(h) ya malengo ya Katiba ya Umoja wa Afrika, na hivyo Ombi hilo lilizingatia Kanuni ya 50(2)(b) ya Kanuni hizo.

Zaidi ya hayo, Mahakama iliamua kuwa lugha iliyotumiwa katika Ombi hilo haikuwa ya kudhalilisha au ya matusi kwa Taifa Lililoshtakiwa au taasisi zake, na hivyo kutimiza Kanuni ya 50(2)(c) ya Kanuni hizo. Ombi hilo pia halikutegemea tu habari zilizosambazwa kupitia vyombo vya habari, kwa kuwa lilitokana na hati za mahakama kutoka mahakama za ndani za Taifa Lililoshtakiwa, na hivyo kutimiza Kanuni ya 50(2)(d) ya Kanuni hizo.

Kuhusu hitaji kwamba Ombi liwasilishwe kwa uda muafaka, Mahakama ilibainisha kuwa uamuzi wa mwisho wa Mahakama ya Rufaa ya Tanzania ulitolewa tarehe 30 Agosti 2019 na Mwombaji aliwasilisha Ombi lake katika Mahakama hii tarehe 15 Novemba 2019, hivi kwamba muda wa miezi kiwili na siku 16 ulikuwa umepita. Mahakama iliamua kwamba muda wa miezi miwili na siku 16 ni muda mwafaka kutokana na maana ya Kanuni ya 50(2)(f).

Mwisho, Mahakama iligundua kuwa kesi hii ilikuwa haijasikilizwa na kuamuliwa hapo mbeleni kwenye mahakama nyingine ya kimataifa na hivyo ilikuwa inazingatia Kanuni ya 50(2)(g) ya Kanuni hizo. Kwa hiyo, Mahakama ilihitimisha kuwa Ombi hilo linakubalika.

Kisha Mahakama iliangalia kama Taifa Lililoshtakiwa lilikiuka haki ya Mwombaji ya kusikilizwa kwa kesi kwa haki, haki yake ya kesi kusikilizwa kwa wakati unaofaa, haki yake ya utu na marufuku dhidi ya mateso, udhalilishaji na unyanyasaji, na haki yake ya uhuru, zilizolindwa katiak Ibara za 7, 7(1)(d), 5 na 6 za Mkataba, mtawalia. Hata hivyo, Mahakama iliona kwamba jambo kuu katika Ombi hilo lilijikita katika Ibara ya 7(1) ya Mkataba, haki ya Mwombaji ya kusikilizwa kwa kesi yake, ambayo inajumuisha haki yake ya kesi kusikilizwa katika muda unaofaa, hivyo, dai hili la ukiukaji ndilo lililoshughulikiwa kwanza.

Mwombaji aliwasilisha malalamiko mawili dhidi ya mahakama za ndani ambazo anadai kwamba vitendo vyake au kutotenda kwake kulikiuka haki zake. Malalamiko haya yanahusu (i) ushahidi ambao ulisababisha upatikanaji wa hatia, na (ii) muda wa kesi katika mahakama za kitaifa.

Katika dai linalohusiana na ushahidi ambao ulisababisha upatikaji wa hatia, Mahakama ilirejelea maamuzi yake ya awali, ambapo ilibainisha kuwa mahakama za ndani zinafurahia kiwango kikubwa cha shukrani katika kutathmini kiwango cha uwezekano wa ushahidi fulani. Kama mahakama ya kimataifa ya haki za binadamu, Mahakama haiwezi kuchukua jukumu hili kutoka kwa mahakama za ndani na kuchunguza utondoti na upekee wa ushahidi unaotumiwa katika kesi za ndani. Hata hivyo, Mahakama inaweza, katika kutathmini jinsi kesi za ndani zilivyoendeshwa, kuingilia kati ili kukadiria kama kesi za ndani, ikiwa ni pamoja na ukadiriaji wa ushahidi, ziliendeha kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya haki za binadamu. Katika kesi hii, baada ya uchunguzi wa kina wa rekodi, Mahakama ilibaini kwamba Mahakama

Ku una Mahakama ya Rufaa zilichukua muda kupitia, kukadiria na kuthibitisha uaminifu wa Ushahidi, likiwemo suala mahusisi la utambulisho wa mashahidi, na zikapata kwamba mashtaka dhidi ya Mwombaji yalithibitishwa pasipo shaka yoyote. Kwa hivyo, Mahakama iliona kuwa jinsi kesi zilizofikishwa katika mahakama ya ndani zilivyoendeshwa, pamoja na uzingatiaji wa ushahidi, hakukuonesha makosa yoyote ya wazi au upotovu wa haki uliohitaji uingiliaji kati. Kwa hivyo, Mahakama ilitupilia mbali madai ya Mwombaji na kuamua kwamba Taifa Lililoshtakiwa halikukiuka haki yake ya kusikilizwa, iliyolindwa katika Ibara ya 7(1) ya Mkataba.

Katika dai lunalohusu haki ya kesi kusikilizwa kwa muda unaofaa, Mahakama ilirejelea uamuzi wake wa awali katika *Wilfred Onyango Nganyi na wengine 9 dhidi ya Tanzania*, ambapo iliamua kuwa "… hakuna muda wastani unaochukuliwa kuwa unaofaa kwa mahakama kukamilisha kesi. Katika kuamua kama muda unafaa au haufai, lazima kila kesi ishughulikiwe kulingana na sifa zake." Mahakama pia ilibainisha kuwa mambo mbalimbali huzingatiwa wakati wa kukadiria kama kesi ilikamilishwa katika muda unaofaa kwa mujibu wa maana ya Ibara ya 7(1)(d) ya Mkataba. Mambo haya yanajumuisha utata wa kesi, mienendo ya wadaawa na mienendo ya mamlaka. Katika kesi hii, Mahakama iliona kuwa Mwombaji alilalamikia muda mwingi uliotumika kukamilisha kesi yake na rufaa pamoja na muda uliopita kati ya kukamatwa kwake na kufikishwa mahakamani. Baada ya kuchunguza vipengele mbalimbali, Mahakama Ilona kwamba muda wa kukamilisha kesi na rufaa ya Mwombaji haukuweza kuonekana kuwa usiofaa na, kwa hivyo, iliamua kuwa Taifa Lililoshtakiwa halikukiuka haki ya Mwombaji ya kesi yake kusikilizwa katika muda unaofaa, iliyohakikishwa katika Ibara ya 7(1)(d) ya Mkataba huu. Kuhusu muda uliopita kati ya kukamatwa kwa Mwombaji na kufikishwa kwake mahakamani, Mahakama ilipata kwamba, katika hali mahususi za kesi hii, muda uliotumika kumfikisha Mwombaji mahakamani ulikuwa unaofaa na, kwa hivyo, ikaamua kwamba Taifa Lililoshtakiwa halikukiuka haki ya Mwombaji ya kesi yake kusikilizwa katika muda unaofaa, inayolindwa katika ibara ya 7(1)(d) ya Mkataba huu.

Kuhusu dai la ukiukaji wa haki ya utu na katazo la kuteswa, kudhalilishwa na kutendewa kinyama, mahakama iliona kuwa Mwombaji alidai kuwa kukamatwa kwake kulikuwa kinyume cha sheria kwa sababu polisi wanadaiwa kutumtesa wakati walipokuwa wanamkamata. Mahakama pia ilitambua kuwa sheria ya Taifa Lililoshtakiwa, chini ya Ibara ya 21 ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya jinai, inawaruhusu maafisa wa polisi kutumia nguvu wakati wa

kumkamata mtu, mradi hakuna nguvu zaidi itakayotumika au kwamba mtu huyo hafanyiwi udhalilishaji mkubwa kuliko inavyotakiwa, ili kumkamata au kuzuia kutoroka kwake baada ya kukamatwa. Mahakama pia ilitambua kwamba sharia ya taifa Lililoshtakiwa, katika Sehemu ya 21 ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya jinai. Mahakama pia ilizingatia, kutoka kwa rekodi, kwamba Mwombaji alijaribu kukwepa kukamtwa kwa kukimbia na kwamba aliendelea kukimbia hata baada ya kupigwa risasi ya onyona kwamba hatimaye alipigwa risasi yamguu ili akamatwe. zaidi ya hayo, Mahakama iliona kuwa Mwombaji hakutoa thibitisho lolote au kufafanua dai kwamba nguvu nyingi zilitumika au kwamba alivunjiwa heshima kuliko inavyostahili wakati wa kukamatwa kwake. Katika hali hizi, Mahakama iliamua kwamba Taifa Lililoshtakiwa halikukiuka haki ya Mwombaji ya utu na katazo la mateso, udhalilishaji na utendewaji kikatili, iliyohakikishwa katika Ibara ya 5 ya Mkataba huu, kuhusu nguvu zilizotumikwa na polisi wakati wa kukamatwa kwake.

Kuhusu dai la ukiukaji wa haki ya uhuru, Mahakama ilibainisha kuwa Mwombaji anadai alikamatwa kiholela, kuzuiliwa katika ulinzi wa polisi na mwishowe kufungwa kwa miaka 30, bila sababu yoyote ya msingi na kwa kuzingatia ukweli usiothibitishwa. Mahakama pia iliona kutoka kwa rekodi na uamuzi wa madai yanayoendela ya ukiukaji wa haki, kwamba Mwombaji hakutoa ushahidi kuonesha na kuthibitisha kwa Mahakama kwamba alikamatwa kiholela, kuzuiwa na kufungwa gerezani, mambo ambayo ni ukiukaji wa haki yake ya uhuru. Katika hali hizi, Mahakama ilipata kwamba hakukuwa na msingi wa kupata ukiukaji na ikaamua kuwa Taifa Lililoshtakiwa halikukiuka haki ya uhuru ya Mwombaji, inayolindwa katika Ibara ya 6 ya Mkataba huu, kuhusu kukamatwa kwake, kuzuiliwa na kufungwa gerezani.

Baada ya kuona kwamba Taifa Lililoshtakiwa halikukiuka haki zozote za Mwombaji, Mahakama ilitupilia mbali maombi ya Mwombaji ya kupewa fidia. Kuhusu gharama, Mahakama iliamua kwamba kila mdaawa ajilipie gharama zake.

Jaji Rafaâ BEN ACHOUR alitoa maoni tofauti, kwa mujibu wa Ibara ya 28(7) ya Protokali na Kanuni ya 70(2) ya Kanuni za Mahakama.

**Taarifa Zaidi**

Taarifa zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na matini kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, inaweza kupatikana kwenye tovuti hapa: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0602019

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa baruapepe registrar@african-court.org

*Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha ulinzi wa haki za binadamu na watu barani Afrika. Mahakama ina mamlaka juu ya kesi na migogoro yote iliyowasilishwa kwake kuhusu ufasiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa haki za binadamu na Wat una hati nyingine yoyote muhimu ya haki za binadamu iliyoidhinishwa na Mataifa yanayohusika. Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu katika www.african-court.org.*